

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)

Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**

30 Machi, 2017

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**Ndugu Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

Ninayo taarifa njema kwetu ya kuwa nchi yetu imepata heshima kubwa ya kutembelewa na Waziri Mkuu wa Ethiopia Mh. **Hailemariam Desalegn** ambaye tunatarajia atafika hapa nchini kwa ziara ya siku mbili kuanzia tarehe 31 Machi – 01 Aprili ,2017 kwa mwaliko wa Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dr John Pombe Magufuli**.

**Ndugu Wananchi,**

Mgeni wetu huyu atakuwa nchini kwa shughuli mbalimbali za kidiplomasia zinazogusa Nyanja za kiuchumi, biashara na ushirikiano baina ya Tanzania na nchi ya Ethiopia.

## **Ndugu Wananchi,**

Tunayo mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa wageni wetu hawa juu ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazolikabili bara la Afrika katika masuala ya kilimo cha kisasa kwa maeneo yenye uoto wa asili wenye changamoto kama milima hapa nchini Tanzania kama ilivyo kwa wenzetu wa Ethiopia ambao mbali ya kukabiliwa na uoto usio rafiki wa milima na miinuko mikali kwa asilimia kubwa bado wameweza kutumia vyema maeneo machache ya tambarare na kuweza kufanya kilimo cha kisasa na kuzalisha chakula kwa wingi.

## **Ndugu Wananchi,**

Kwa kutambua ugeni huu sisi kama wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania tunamkaribisha mgeni wetu na ajisikie nyumbani muda wote atakapokuwa hapa jijini. Tutambue kuwa ujio wowote ule huwa unakuja na kheri na unafungua mambo mengi kwa ajili yetu.

Asanteni sana.

Paul C. Makonda

**MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

**30/03/2017**